# RAMOVIC ASHITUKIA MCHEZO YANGA

kumekucha @kumekucha @kumekucha

mwanzo mpya

# KUMEKUCHA

Tovuti: Tovuti www.kumekucha.co.tz/ ISSN 4562-9710. NA. 07, Jumatano Januari 22, 2025 Bei Tsh. 1,000/= Ksh 100

# MBOWE,LISSU KESI IMEISHA!

- WAMALIZA TOFAUTI ZAO HADHARANI, KURA ZAPIGWA USIKU MNENE,WAJUMBE WAGAWANYIKA



## TRUMP AFUTA URAIA WA KUZALIWA KWA WAHAMIAJI



## WIZARA YA MADINI YAKUSANYA BILIONI 521

## DK.BITEKO-MITAALA IENDANE NA MABADILIKO YA TEKNOLOJIA

# MBOWE,LISSU KESI IMEISHA!

NA HUSNA NASSORO

HOTUBA zilizotolewa na wagombea wa nafasi ya Uenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA)Tundu Lissu na Freeman Mbowe katika Mkutano Mkuu wa uchaguzi uliofanyika jana zimewashtua wengi baada ya kuonesha kujaribu kuponya majeraha ya kampeni baina ya wawili hao.

Itakumbukwa kabla ya zoezi la uchaguzi huo jana wagombea hao walikuwa katika mnyukano mkali wa kurushiana kashfa na maneno makali yaliyoibua sintofahamu ya hatima ya chama hicho baada ya uchaguzi.

Hotuba za wagombea hao ni kama zilionesha kuwakuna wajumbe wa Mkutano huo ambao hawakutarajia kusikia maneno ya mshikamano kwa maslahi ya chama hicho kutokana mnyukano wa kampeni ulivyokua.

CHADEMA imefanya uchaguzi wa viongozi wake wa ngazi ya taifa huku nafasi ya Mwenyekiti wa chama ikigombaniwa na watu watatu,Freeman Mbowe,Tundu Lissu na Odero Charles Odero lakini mchuano ulikuwa mkali zaidi kati ya Mwenyekiti anayemaliza muda wake na Makamu.

Katika hotuba yake mbele ya wajumbe wa Mkutano Mkuu, Lissu alisema,

licha ya kutofautiana kimtazamo na Mwenyekiti wake Mbowe lakini hawajawahi kugombana akiamini hali hiyo itaendelea hata baada ya uchaguzi huo.

"Nimekaa pembeni ya Mwenyekiti wetu wa Chama mfululizo kwa miaka zaidi ya 20 na katika kipindi chote hicho hatujawahi kugombana,hatujawahi kupigana mimi na yeye binafsi,tumetofautiana kimsimamo lakini hatujawahi kugombana.Sijawahi kuwa na ugomvi na mwenyekiti na natumaini hili litaendelea baada ya mshindi kutangazwa,"alisema Lissu.

Alisema,hata mara baada ya uchaguzi ataendelea kuwepo ndani ya Chadema ili kuendeleza ujenzi wa chama hicho huku akihimiza umoja baina ya wanachama wa chama hicho.

Kwa upande wake Mbowe,alisema,baada ya uchaguzi atahakikisha wanafanya maridhiano ili kuponya majeraha yaliyotokana na uchaguzi akifafanua atakua tayari kumpa ushirikiano mshindi ili kuijenga

**Chadema.**

Alisema,kwake umoja baina ya wanachama wa chama hicho na hatima ya kesho ya CHADEMA ndiyo jambo muhimu kuliko kitu kingine.

Zoezi la upigaji kura lilichelewa kuanza kutokana na uhakiki wa wajumbe kuchukua muda mrefu hatua iliyofanywa mambo kuendelea hadi usiku mnene ambapo hadi gazeti hili linakwenda mitamboni mambo yalikuwa bado hayajaanza.

Wababe hawa wawili katika siasa za chama hicho wanaitaka nafasi ya uenyekiti katika mbio hizo ambapo mambo mengine yamezuka kwa faida ya chama na mengine yanaonekana kukiumiza chama.

## DKT.BITEKO ATAKA MITAALA IENDANE NA MABADILIKO YA TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

VYUO na taasisi zinazotoa elimu ngazi ya Kati ikiwemo Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE),zimetakiwa kuboresha mitaala yake ya masomo ili iendane na mahitaji ya sasa ya soko la ajira kimataifa sambamba na mahitaji ya kijamii na kiuchumi.

Hayo yamebainishwa jana na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko katika Maadhimisho ya miaka 60 ya chuo hicho kilichoanzishwa Januari 21, 1965.

"Serikali inasisitiza matumizi ya teknolojia za kisasa na mbinu za kujifunza zinazojibu changamoto za kimataifa, " Amesema Dkt. Biteko.

Amesema kuwa Serikali inazitaka taasisi za elimu ya kati kikiwemo Chuo cha CBE kuweka mkazo kwenye mafunzo ya ujasiriamali, ili wahitimu wake waweze kuchangia kikamilifu katika uchumi wa taifa kupitia biashara bunifu na ajira binafsi.

Aidha, taasisi za elimu, zikiwemo vyuo kama CBE, amezitaka kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira na pia kusaidia kukuza sekta hiyo kwa utafiti na mafunzo.

Ameongeza kuwa, Serikali inahimiza vyuo vya elimu ya biashara kufanya tafiti za kina zinazosaidia kutatua changamoto za kiuchumi, kuimarisha sera za biashara, na kubuni suluhisho endelevu.

Naye, Waziri wa Viwanda na Biashara,Selemani Jafo amesema CBE ni kitovu cha biashara nchini na kimeweza kujenga mahusiano na nchi mbalimbali kimataifa ikiwemo nchi ya China na Ujerumani na ni ufunguo wa ufanyaji wa biashara katika kampasi zote nchini.

Kwa upande wake, Waziri wa Fedha,Dkt. Mwigulu Nchemba amesema CBE imekuwa ikifanya kazi nzuri na kina mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta ya fedha hapa nchini.

"Fedha na Biashara na Uwekezaji havitengamani lakini mafanikio yote yaliyofikiwa lazima tumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono na uongozi wake uliotuheshimisha, " Amesema Mhe. Nchemba.

Vile vile, Mkuu wa Chuo cha CBE, Prof. Edda Lwoga amesema kuwa katika maadhimisho ya miaka 60 ya CBE wemekuwa wakitoa elimu ya biashara kwa makundi mbalimbali ya kijamii na pia wametoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali wa biashara.

## TRUMP AFUTA URAIA WA KUZALIWA KWA WAHAMIAJI

BBC

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesaini amri kadhaa za kiutendaji baada ya kuapishwa, ikiwemo kufuta haki ya uraia wa kuzaliwa kwa watoto wa wahamiaji haramu na wenye viza za muda.

Uamuzi huu umebadilisha tafsiri ya muda mrefu ya marekebisho ya 14 ya Katiba ya Marekani, ambayo yalikuwa yakitoa uraia wa kuzaliwa kwa yeyote aliyezaliwa nchini Marekani, bila kujali hali ya kisheria ya wazazi wake.

Kwa mujibu wa amri hiyo mpya, watoto waliozaliwa Marekani hawatatambuliwa kama raia wa nchi hiyo iwapo wazazi wao ni wahamiaji wasio halali au wana viza za muda.

Hatua hiyo itaanza kutekelezwa siku 30 kutoka sasa, na watoto watakaozaliwa nchini humo watahitajika kuwa na angalau mzazi mmoja ambaye ni raia wa Marekani au mkazi wa kudumu mwenye kadi ya kijani.

Marekebisho ya 14 ya Katiba ya Marekani, yaliyopitishwa zaidi ya karne moja iliyopita, yamekuwa msingi wa uamuzi wa Mahakama ya Juu yanayowalinda watoto wa wazazi wa kigeni waliozaliwa nchini Marekani.

## WATUHUMIWA KESI YA UHUJUMU UCHUMI WARUDISHWA RUMANDE

NA MWANDISHI WETU

VIJANA sita wanaokabiliwa na mashtaka 68 ya uhujumu uchumi, yakiwemo madai ya kufanya udanganyifu kwa kutumia mashine za kielektroniki za utoaji risiti (EFD), na kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya shilingi bilioni 2.1, wanaendelea kusota rumande kutokana na upelelezi wa kesi yao kutokukamilika.

Waliofikishwa mahakamani ni Stanslaus Mushi (27), mfanyabiashara mkazi wa Malamba Mawili, Nemence Mushi (29), Rose Nanga (33) ambaye ni mhasibu wa soko mkazi wa Kimara B, Hussein Mlezi (37) fundi wa kompyuta mkazi wa Mbagala Kuu, Edwin Mark (22) mkazi wa Yombo Vituka, na Salim Salehe (45) mchoraji.

Mashtaka yanayowakabili yanahusisha matumizi mabaya ya mashine za EFD kwa lengo la kupotosha mfumo wa TRA, pamoja na upatikanaji wa namba za utambulisho wa mlipakodi (TIN) na usajili wa Ongezeko la Thamani (VAT) kwa njia ya udanganyifu.

Wakili wa Serikali, Rhoda Maingu, akisaidiana na Wakili Auni Chilamula, aliieleza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni mbele ya Hakimu Mkazi Amos Rweikiza kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.



# SERIKALI IMEFANYA UWEKEZAJI MKUBWA KWA TMA-MAJALIWA

NA MWANDISHI WETU

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini ikiwemo upande wa miundombinu ya uangazi wa hali ya hewa na kujenga uwezo wa wafanyakazi.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa,alipozindua Mradi wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani wa "Systematic Observation Financing Facility (SOFF) - Project" katika Ukumbi wa Hotel ya Midland Inn View, Dodoma.

Majaliwa amesema lengo la Serikali la kuendelea kufanya maboresho hayo ni kuwezesha utoaji wa utabiri wa hali ya hewa na tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa.

Amesema miongoni mwa uwekezaji huo ni ununuzi wa rada saba za hali ya hewa, upanuzi wa Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa na uboreshaji wa vifaa vya hali ya hewa kwa kuondoa vifaa vinavyotumia zebaki kwa mujibu wa matakwa ya Mkataba wa Minamata.

Waziri Mkuu amesema, Serikali ya Tanzania katika kuunga mkono utekelezaji wa mradi wa SOFF imetenga fedha za kununua Vituo 11 vya Hali ya Hewa. Vituo hivyo vinavyojiendesha vyenyewe vitachangia data katika Mtandao wa Kimataifa wa Uangazi.

Pia, Waziri Mkuu amesema Serikali inaunga mkono kwa kutoa mchango wa zaidi ya dola za Marekani milioni nne ambazo ni thamani ya mchango kwa njia ya huduma zisizo za kifedha (In-Kind contribution). "Jitihada zote hizo, zinaonesha dhamira ya dhati ya Serikali katika kuboresha miundombinu ya hali ya hewa."

Akizungumzia kuhusu uzinduzi wa mradi wa SOFF "SOFF - Investment Phase Project", Mheshimiwa Majaliwa amesema mradi huo una umuhimu mkubwa siyo tu kwa kukidhi mahitaji ya data za hali ya hewa na tabianchi kwa ajili ya utabiri wa hali ya hewa duniani, bali pia kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu ya Tanzania.

Amesema hatua hiyo inalenga kuimarisha upatikanaji na ubadilishanaji data za hali ya hewa kimataifa, hivyo kuimarisha huduma za hali ya hewa na tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa. "Mafanikio katika utekelezaji wa SOFF yatachangia sana kuimarisha ustahimilivu wa matukio ya hali mbaya ya hewa kwa maendeleo endelevu nchini".

Amesema kuwa uchumi wa nchi nyingi zinazoendelea unategemea sana sekta zinazohusiana moja kwa moja na hali ya hewa, ambazo ni kilimo, lakini pia, ufugaji, nishati, maji, afya, madini na usafirishaji.

# WIZARA YA MADINI YAKUSANYA BILIONI 521

MWANDISHI WETU
Dodoma,

WIZARA ya Madini imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 521 katika kipindi cha Julai 1, 2024, hadi Desemba 31, 2024. Hii ni sawa na asilimia 52.2 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 1 kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Madini, Mhe. Anthony Mavunde,jana jijini Dodoma wakati akiwasilisha Taarifa ya utekelezaji ya Wizara mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Waziri Mavunde amesema mafanikio hayo yanatokana na usimamizi mzuri, udhibiti madhubuti, na weledi katika ukusanyaji wa mapato kwenye sekta ya madini.

"Wizara imepiga hatua kubwa ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2015/16 ambapo ilikusanya shilingi bilioni 161 kwa mwaka mzima na mwaka huu ndani ya nusu ya kwanza tayari tumekusanya asilimia 52.2 ya lengo la Shilingi trilioni 1 kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/25".

Katika hatua nyingine, Waziri Mavunde ameongeza kuwa leseni kubwa na za kati za madini ambazo hazijaendelezwa zitarudishwa Serikalini zitakabidhiwa kwa Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) kwa ajili ya

Aidha,Mavunde amesema kuwa, STAMICO imejipanga kuwa sehemu muhimu ya uzalishaji wa Madini ya Kinywe hapa nchini ikiwa ni sehemu ya juhudi za Tanzania kuwa kiungo muhimu katika soko la dunia la madini hayo.



# MHANDISI MAHUNDI ACHANGIA MIL.2 KIKUNDI CHA VICOBA

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya amechangia shilingi milioni mbili kwa kikundi cha VICOBA Ivima cha Makongolosi Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya kwa ajili ya ukamilishaji wa ukumbi wa mikutano.

Mbali ya kuchangia pesa hiyo Mahundi amekipongeza kikundi hicho chenye wanachama thelathini kwa namna kinavyopiga hatua kwa kuwa na miradi mingine kama kioski cha maji na maduka.

Awali Besta Masika katibu wa Kikundi hicho amesema wanahitaji shilingi milioni hamsini ili kukamilisha ujenzi wa ukumbi huo utaosaidia ufanyikaji wa mikutano kwa wakati.

Masika amesema changamoto inayowakabili ni pamoja na baadhi ya wanachama kutorejesha mikopo kwa wakati.



# UMEME 'WAUNAJISI' MKUTANO MKUU CHADEMA



NA HUSNA NASSORO

MKUTANO Mkuu wa Mkuu wa uchaguzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) uliofanyika jana uliingia dosari baada kutokea kadhia ya kukatika kwa umeme zaidi ya mara nne wakati wagombea wa nafasi ya Uenyekiti wakiongozwa na Tundu Lissu wakihutubia wajumbe.

Mkutano huo uliofanyika katika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam ambapo umeme ulikatika ghafla wakati Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, akitoa neno lake la shukrani kwa Wanachama wa CHADEMA kabla ya kuanza kwa mchakato wa upigaji kura.

Baada ya muda mfupi umeme umerejea na Lissu akaendelea kuhutubia ambapo alisikika akisema "Tutafika tu" lakini tukio likatokea tena na kufanya wajumbe wa mkutano kuonesha kuchukizwa na menejimenti ya ukumbi huo.

Baada ya kutokea kwa kadhia hiyo Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, akawatangazia Wajumbe wa Mkutano Mkuu kuwa kwa sasa watatumia jenereta badala kutumia umeme wa kawaida kuepusha kukatika katika kwa umeme mpaka mwisho wa mkutano.



# JE, WAJUA CHANZO NA DALILI ZA KUKOSA NGUVU ZA KIUME?



Jimmy Charles

Uume kulegea maana yake ni uume kutokuwa na uwezo wa kusimama na kushindwa kufanya tendo la ndoa. Kupatwa na tatizo la kuishiwa nguvu za kiume mara kwa mara hupoteza sifa za muhusika. Ikiwa kama hali hii itadumu kuendelea, hivyo inaweza kusababisha msongo wa mawazo, huharibu ujasili wako na huchangia kukaribisha matatizo katika mahusiano ya ndoa.

**Dalili Zake**

Kwa kawaida dalili za kuishiwa na nguvu za kiume huwa kama ifuatavyo:

Uume kushindwa kusimama

Uume kushindwa kufanya tendo la ndoa

**Kukosa hamu ya tendo la ndoa**

Na ieleweke kuwa, tatizo hili linapojitokeza tafadhali muhusika anapaswa kumuona daktari mapema. Muone daktari ikiwa kama:

Una matatizo ya kuwahi ama kuchelewa kufika kileleni

Una ugonjwa wa kisukari, moyo au magonjwa mengine yasiyofahamika ambayo yanaweza kuambatana na hali ya kuishiwa nguvu za kiume.

Una dalili zingine ikiwa pamoja na kupungukiwa nguvu za kiume

**Visababishi Vyake**

Hamu ya tendo la ndoa kwa mwanaume huwa ni njia isiyoelezeka inayohusisha ubongo, vichochezi(hormones), hisia, neva za fahamu, misuli pamoja na mishipa ya damu. Kupungukiwa nguvu za kiume kunaweza kuwa ni matokeo ya mojawapo ya matatizo magonjwa. Vile vile, msongo wa mawazo, pamoja na afya katika mfumo wa fahamu kunaweza kuwa kisababishi ya kupungukiwa nguvu za kiume.

Wakati mwingine matatizo ya kimwili na kiakili husababisha nguvu za kiume kupungua. Kwa mfano, hali mbaya ya kimwili inayoweza kusababisha hamu ya tendo la ndoa kutoweka inaweza kuleta wasiwasi juu ya kutengeneza nguvu za uume kusimama. Hali ya mashaka na wasiwasi unaojitokeza unaweza kusababisha uume kushindwa kusimama.

Je, Ni Matatizo Gani Ya Kimwili Yanayosababisha Kukosa Nguvu Za Kiume?

Katika mambo mbalimbali, upungufu wa nguvu za kiume umekuwa ukisababishwa na matatizo ya kimwili. Vyanzo vyake ni pamoja na:

Magonjwa ya moyo

Damu kuganda kwenye mishipa ya damu

Mkusanyiko wa mafuta kwenye damu(High Cholesterol)

Shinikizo la juu la damu(High Blood Pressure)

Kisukari

**Unene na kitambi pia**

Mafuta kujaa kiunoni

Matumizi ya ugoro ama tumbaku

Kupiga punyeto muda mrefu

Ulevi wa pombe kama vile viloba, bia, nk

**Kukosa usingizi**

Kuvimba kwa tezi dume

Matatizo yanayokuwa kwenye uti wa mgongo

Je, Ni Matatizo Gani Ya Kiakili Yanayosababisha Kukosa Nguvu Za Kiume?

Ubongo huchangia sehemu kubwa katika kuamsha viungo vya uzazi ili kupata hisia kama vile nyege, na kuufanya uume kuweza kusimama. Lakini yapo mambo mengi yanayoweza kuingiliana na hisia za kimapenzi na zinaweza kusababisha nguvu za uume kupungua. Mambo haya ni kama yafuatayo:

Mashaka, wasiwasi au hali nyingine ya afya ya ubongo

Msongo wa mawazo kutokana na sababu mbalimbali kama vile mambo ya kiuchumi, kuachwa na mwezi wako, madeni, magonjwa,kutengwa na ndugu, mahusiano kuvunjika, nk

**Je, Kuna Vihatarishi?**

Na ieleweke kuwa, kadiri mwanaume umri wake unapozidi kuwa mkubwa, uume wake huchukua muda mrefu kusimama(yaani kudindisha) na kuwa imara au kukaza zaidi kama alivyokuwa kijana. Itampasa muda mwingi kutumia kuupapasa uume wake ili uweze kusimama.

Yapo mambo mbalimbali yanayoweza kuchangia kuwa vihatarishi na kufanya uume kuishiwa nguvu, nayo ni:

Matumizi ya madawa ya vidonge kwa muda mrefu kutokana na tiba za magonjwa ya moyo au kisukari

Matumizi ya tumbaku ambayo huzuia mtiririko wa damu kuingia katika mishipa ya fahamu au moyo.

Kuwa na uzito mkubwa wa kupindukia, hasa unene

Ajali ikiwa kama uliipata ikaharibu mishipa ya fahamu

**Tahadhari**

# ASILI YA UGOMVI WA EDWARD LOWASSA NA SAMUEL SITTA





MWAKA 1995, ilianza misheni ya kumshawishi Dk Salim Ahmed Salim, aachane na ukatibu mkuu wa OAU, arejee kuchukua fomu ya kugombea urais kupitia CCM.

Misheni hiyo ilipofeli, wazee, Mwalimu Nyerere na Mzee Rukhsa, walimketisha Jakaya, wakamshawishi achukue fomu. Jakaya akawa anasita. Hakujiamini.

Mtu wa mipango, Edward Lowassa, aliusoma mchezo, akaupa tafsiri chanya. Akampa somo kaka mkubwa, Samuel Sitta. Ikawa timu. Edward na Sitta, wakamwendea Jakaya. Wakamshawishi achukue fomu.

Tofauti na ushawishi wa wazee kwa Jakaya, safari hii Edward na Sitta, walibeba ramani ya upacha. Jakaya na Edward waingie ulingoni kama mapacha. Ambaye angekwama njiani, angemsaidia mwenzake ashinde. Sitta akawa meneja kampeni.

Edward na Sitta, walimhakikishia Jakaya kuwa wangemfanyia kila kitu. Jakaya alikuwa Waziri wa Fedha. Alitingwa na maandalizi ya bajeti ya Serikali 1995-1996. Edward na Sitta, walizungusha fomu ya Jakaya nchi nzima, ikapata wadhamini. Jakaya akiwa zake ofisini, Dar.

Huo ndiyo ulikuwa mwanzo wa ndoa ya kisiasa ya Jakaya na Edward. Sitta ni mhusika muhimu. Watu hao watatu, jumlisha Rostam Aziz, aliyeingia baadaye, ndiyo vichwa vikuu vya mtandao ulioshinda kiti cha urais mwaka 2005. Jakaya akaingia Ikulu.

Ajabu, miaka mwili baada ya ushindi wao, walivurugana. Moto uliwaka bungeni. Edward alitoswa uwaziri mkuu kupitia "ajali" ya Richmond, Sitta akiwa Spika wa Bunge.

Edward akasema: "Tatizo ni uwaziri mkuu."

Eti, Sitta alimwonea kijicho Edward kuwa waziri mkuu. Kwa nini na walikuwa timu moja?

Jibu ni hili; wanamtandao walikuwa desperate kuhakikisha Jakaya anashinda urais 2005. Mizungu mingi ilichezwa kupitia kanuni: "Sema Chochote, Kubali Chochote, Ahidi Chochote, Chafua Yeyote, Mradi Jakaya awe Rais."

Kanuni hiyo ndiyo asili ya mgogoro wa Edward na Sitta. Wote waliahidiwa uwaziri mkuu. Edward akapata, Sitta akatakiwa awe Spika wa Bunge.

Kitabu changu cha "Kikwete Lowassa; Urafiki, Ndoa Yao ya Kisiasa, Uadui", kina mengi. Kinapatikana TPH Bookshop, House of Wisdom na Elite Bookstore.

Unaweza kukipata popote ulipo kwa kupiga simu namba +255787616381 au +255713355717.

**Bei ni Sh75,000.**
**Ndimi Luqman MALOTO**



# NIMEANZA KUKITAFUTA KITABU CHA EDWARD LOWASSA

NA VICTOR MAKINDA

KITABU cha Waziri Mkuu mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Edward Ngoyai Lowassa, kimefungwa rasmi mchana wa Februari 17,2024 kijijini Ngarashi, wilayani Monduli Mkoani Arusha.

Lowassa ametuachia kitabu chenye kurasa nyingi zilizojaa, furaha, tabu na mahangaiko. Zipo pia kurasa zinazotoa elimu, maarifa na ujuzi kwa msomaji.Kitabu kilichofungwa cha Lowassa kina kurasa zilizosheheni, maanguko, furaha na mafanikio. Kitabu cha Lowassa kimefungwa kikiwa na simulizi tamu za kusisimua, zenye mafunzo mithili ya mafunzo ya jandoni.

Kitabu hicho ukikisoma, unaweza pia kububujikwa na machozi, kutiwa moyo na hata kukata tamaa. Jambo la kufurahisha zaidi kitabu cha Lowassa, kina kurasa ambazo zinafunza kinaga ubaga, na kutia ari ya kupambana, kusamehe kukusanya makundi ya watu wa rika na hadhi mbali mbali kutoka kwenye jamii na makabila tofauti tofauti.

Pamoja na mambo mengine, kitabu kinafundisha umuhimu wa bidii, uaminifu, juhudi na kujitoa kwa ajili ya wengine. Kitabu kinafundisha kutokuwa mchoyo, mlafi na mbinafsi. Kitabu cha Lowassa hakiachi kufundisha misimamo thabiti na kusimamia hoja zenye maslahi mapana kwa jamii kwa ajili ya ustawi wa jamii.

Yapo mengi, lakini pia kitabu kinafundisha umuhimu wa amani, umoja, mshikamano na uzalendo kwa Taifa kwa Taifa.Wengi wameandika mengi kuhusu mtu huyu aliyejizolea umaarufu mkubwa ndani na nje ya mipaka ya nchi kana kwamba alikuwa kiongozi wa Taifa. Ninamaanisha Rais wa Jamhuri.

Lah hasha, Lowassa hajawahi kushika wadhifa huo mkubwa wa urais bali aliishia kwenye uwaziri mkuu tu na tena alihudumu kwa muda usiozidi miaka miwili. Aligombea urais kupitia chama cha upinzani lakini kura zake hazikutosha. Toka wakati huo hajawahi kushiriki kwenye majukwaa ya siasa za moja kwa moja, akabaki kimya mpaka siku tulipotangaziwa kuwa amefariki dunia.

Pamoja na ukimya wake kwenye majukwaa ya kisiasa lakini alibaki mioyoni mwa watanzania.

Kwa nini basi kitabu chake kifungwe kwa maandamano, sherehe zilizohudhuriwa na umati mkubwa wa watu?

Kwa nini sasa mara baada ya kufumba macho, watu wote wa chama chake na wasio wa chama chake, wake kwa waume, vijana kwa wazee wote waoneshe kuguswa na kuumia mioyoni kila mmoja kwa namna yake na hata kumwagia sifa kemkem? Jibu ni rahisi mno. Lowassa kama walivyosema wengine alikuwa mtu wa watu aliyewafikia watu na kuruhusu watu wamfikie kirahisi na kwa namna ya pekee kabisa. Hakuwa mbaguzi, aliwapenda watu na alikuwa mwepesi wa kuwasamehe wote waliomkwaza.

Imeandikwa kwenye vitabu vitakatifu kuwa usipokuwa mwepesi wa kusamehe utakua na maadui wengi sana. Lowassa, alikuwa mwepesi wa kusamehe. Sitaki kuamini kuwa hakuwahi kukwazwa, kuudhiwa na kuchukizwa na watu wote aliokuwa karibu nao.

Siku ya kufunga kitabu chake inadhihirisha kuwa mtu huyu alikuwa mwepesi wa kusamehe ndio sababu hakuwa na maadui zaidi ya lundo la marafiki waliomwaga machozi huku wakiziimba sifa zake njema.

Zawadi ya maisha ya Lowassa ni kwa waliobaki hai. Kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kutafakari kwa kina ni namna gani anaweza kuishi maisha ambayo Lowassa aliyaishi. Anapaswa kutafakari mafunzo ambayo yanapatikana katika kitabu cha Lowassa na kuyaishi.

Lowasa katika maisha yake hapa Duniani, aliwahi kufanya kazi kwa ukaribu na watu wenye shari na wapenda vurugu. Watu hao walifikia hata hatua ya kumshawishi atangaze maandamano ambayo nina hakika kuwa ikiwa yangelifanyika, nchi ingeingia katika hali ya sintofahamu na vurugu kubwa.

Lakini kwa kuwa Lowassa alikuwa muumini wa amani, aliyechukia vurugu, hakufanya kama walivyotaka washirika wake, bali alitumia hekima ya hali ya juu, kuwatuliza wapenda vurugu hao na kuwatuliza wanachama kwa ujumla na hatimae kuiepusha nchi kuingia kwenye sintofahamu.

Huyo ndiye Lowassa ambaye kitabu cha maisha ya uhai wake kinapaswa kusomwa na kila mzalendo wa nchi hii kwani kina mafunzo makubwa katika kulijenga Taifa la kistaarabu.

Kila mmoja ajiulize swali je ikiwa atakufa leo, atazikwa kama Lowassa alivyozikwa? Swali kubwa zaidi libaki kuwa, kwa kuwa maisha yetu ni hadithi, ni kitabu cha simulizi, je tutakaao waacha baada ya sisi kutangulia wakisoma kuhusu maisha yetu watajifunza nini?



# VIATU VYA MGOMBEA MWENZA VINAMTOSHA

NA BWANKU M BWANKU.

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM)kinachoongoza Taifa Tanzania kimekua na wiki ya aina yake kuanzia Jumamosi na Jumapili Januari 18 na 19, 2025 kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.




CCM ulikua ni Mkutano Mkuu wake Maalum ambao ulikua na ajenda mbalimbali kubwa ikiwa kumchagua Makamu Mwenyekiti wa Chama hicho baada ya aliyekua akishika nafasi hiyo Ndugu Abdulrahman Kinana kujiuzulu,hatimaye Ndugu Stephen Masatu Wasira akachaguliwa kuziba nafasi hiyo.

Kwenye Mkutano Mkuu huu Maalum licha ya ajenda zake Mama zilizokua zinajulikana na shughuli zilizofanyika kama hiyo ya kumchagua Makamu Mwenyekiti, kupokea taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Chama na mabadiliko madogo kwenye Katiba yake.

Pia kumpitisha Rais Samia Suluhu Hassan kuwa Mgombea Urais wa CCM na Dkt. Hussein Mwinyi kuwa Mgombea Urais wa CCM Zanzibar, Mkutano huu umefanya jambo lingine kubwa ambalo halikutarajiwa na yeyote na kutikisa Taifa wakati huu kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu hapo baadae.

Kwa mshangao mkubwa, bila kujulikana wala kutarajiwa na yeyote, hatimae Mkutano Mkuu huu umemthibitisha Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kuwa Mgombea Mwenza wa CCM wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu 2025.

Hili linatokea baada ya Makamu wa Rais Dkt.Philip Mpango na ambaye alitarajiwa kuwa Mgombea Mwenza wa Dkt.Samia kwenye Uchaguzi Mkuu kuomba na kuandika barua kwa Rais Samia ya kupumzika.

Hatimaye ndani ya Mkutano huo kikafanyika kikao cha haraka haraka cha Kamati Kuu ya CCM ambacho kilikuja na jina la Dkt.Nchimbi na Mkutano Mkuu kumthibitisha papo hapo. Hakuna aliyetarajia, Taifa limepata mshangao mkubwa sana.

Imekua ghafla na historia bila ya kutarajiwa na yeyote CCM kwenye Mkutano Mkuu wake huu ambao hata haukua na ajenda hiyo kumpata Mgombea Mwenza atakayesimama na Rais Samia kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka huu 2025 ambaye ni Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi.

Sasa, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi ni nani?

Jina la Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi sio jina geni kwenye anga la siasa za Tanzania. Ni moja ya wanasiasa wakubwa, mahiri na wakongwe wanaoendelea kuteka uga huu wa siasa za Tanzania.

Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi ni moja ya wanasiasa wakubwa sana kwenye siasa za Tanzania. Kwa utumishi na uzoefu wake mkubwa ndani ya CCM na serikali akiwa na zaidi ya miaka 35 akishika nafasi kubwa na nyeti za maamuzi.

Ndiye Katibu Mkuu wa CCM kwasasa, Chama kinachoongoza Taifa hili. Ameshika nafasi mbalimbali kwenye ngazi za chini na za msingi za CCM,akiwa Chuo mwaka 1997 alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC)na mwaka mmoja mbele 1998, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Jumuiya aliyoiongoza mpaka mwaka 2008.

Pia amewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Bunda iliyoko mkoani Mara wakati wakati wa Awamu ya 3 ya Hayati Benjamin Mkapa kuanzia mwaka 2003 hadi 2005.

Kuwa Kiongozi Mkuu wa Jumuiya hiyo ya Vijana kwa ngazi ya Taifa, moja kwa moja kukampa tiketi ya kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM na Halmashauri Kuu (CC & NEC).

Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya CCM ni moja ya vikao vya juu kabisa vitatu vya CCM kando ya Mkutano Mkuu wa CCM Taifa ambavyo vinafanya maamuzi makubwa ndani ya Chama hicho ikiwemo kumpitisha Mgombea Urais wa CCM, Mwenza,Wabunge lakini vikiwa ni vikao vinavyojadili hali ya CCM na utekelezaji wa Ilani yake na serikali na mengine mengi makubwa yanayogusa maslahi ya Taifa zima.

Baada ya kuhudumu kwenye nafasi kubwa ndani ya Chama na zenye maamuzi makubwa ndani ya Chama na Taifa, Mwaka 2005 Dkt. Nchimbi aligombea Ubunge kwenye Jimbo la Songea Mjini na kushinda ambapo moja kwa moja Rais wa Awamu ya 4 wa kipindi hicho Dkt.

Jakaya Kikwete alimteua kuwa Naibu Waziri kwenye Wizara 3 akianza kuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kuanzia Januari 2006, kisha Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana mwaka huohuo Oktoba pamoja na Naibu Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alikohudumu kuanzia Februari 2008 hadi 2010 kwenye Uchaguzi Mkuu.

Mwaka 2010 aligombea tena na kushinda na hapo sasa Rais wa Awamu ya 4 Dkt. Jakaya Kikwete akamteua kuwa Waziri kamili akianza kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo na baadae Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mwaka 2016, Dkt. Nchimbi aliteuliwa na Aliyekuwa Rais wa Awamu ya 5 Hayati John Magufuli kuwa Balozi wa Tanzania nchini Brazil kabla ya baadae mwaka 2022 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kumbadilishia Kituo cha kazi ya Ubalozi kwa kumteua kuwa Balozi wa Tanzania nchini Misri, nafasi aliyohudumu mpaka mwaka Jana 2023 alipomaliza muda wake na kurudi nchini kwa mujibu wa sheria.

Baada ya kazi kubwa akianzia ngazi za chini za uongozi, Uenyekiti wa Jumuiya ya Vijana Taifa (UVCCM), Mbunge, Naibu Waziri hadi Waziri kamili na Ubalozi hatimaye Januari 15, 2024 Dkt. Nchimbi aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM, Mtendaji Mkuu wa Chama hiki kinachoongoza Taifa letu Tanzania

Anasifika kwa misimamo madhubuti isiyoyumba (hili nitalichambua) akiwa na ushawishi mkubwa ndani ya Chama na Nje hasa kwa kufanya kazi ndani na Nje ya Nchi. Kwa CV yake hii ilivyoshiba akishika nafasi kubwa na nyeti akianzia ngazi za chini, ni mtu madhubuti kuweza kuwa msaidizi namba moja wa Mkuu wa Nchi.

Ni ukweli usiopingika kwamba kwa Rais kariba ya Dkt. Samia anayefanya mageuzi makubwa ya maendeleo ndani ya nchi anahitaji kuwa na wabobezi wakubwa wa siasa na utumishi kumsaidia kutafsiri maono yake.

Balozi Nchimbi ni Msomi mzuri aliyebobea kwenye masuala ya Fedha na Benki akihitimu Shahada ya Uzamivu (PHD) kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe mwaka 2011.

# RAIS SAMIA ANATUPELEKA NCHI YA AHADI

NA VICTOR MAKINDA

"MATAMANIO ya binadamu siku zote ni kuona anakuwa bora zaidi leo kuliko jana. Hadithi katika vitabu vitakatifu zinasimulia kuhusu ahadi ambazo wana wa Israel walipewa ya kuwa watakwenda kuishi nchi ya ahadi itakayokuwa na maziwa na asali.

Siku zote binadamu hufanya jitihada kuhakikisha kuwa anapambana na changamoto zinazo mkabili ili aishi kwenye eneo ambalo lina mahitaji yote yanayohitajika kwa ajili ya ustawi wake. Viongozi mahali pengi duniani wamekuwa wakihangaika usiku na mchana kushirikiana na wananchi wanaowaongoza kuhakikisha kuwa wanapambana na changamoto mbali mbali zinazokabili katika jamii.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ni kiongozi ambaye uongozi wake unatoa tafsiri na taswira ni mtu anayetamani kuona wananchi wake wanaishi maisha yanayofanana na yale ya nchi ya ahadi."

Hayo ni maneno ya Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC)kupitia Jumuiya ya Wazazi Taifa,Hamoud Abuu Jumaa ambaye ni Mbunge wa zamani wa Kibaha Vijijini.

Hamoud ambaye bado ni kipenzi cha Wana Kibaha kutokana na mambo makubwa aliyolifanyia jimbo hilo kabla ya kuenguliwa katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ameliambia KUMEKUCHA,kuelekea miaka minne ya Rais Samia madarakani ni wazi serikali yake imeonesha mwelekeo wa safari ya maisha ya watanzania kuelekea nchi ya ahadi kutokana na hatua kubwa za maendeleo zinazofikiwa.

"Miaka minne ya Rais Samia madarakani imedhihirisha kwanza kuwa wanawake wana uwezo mkubwa wa kiuongozi na wakiipata fursa ya kuongoza huongoza vizuri kwa kufuata dira na muelekeo sahihi wa maendeleo." anasema.

Hamoud anasema kuwa katika uga wa maendeleo Rais Samia ameonesha jitihada kubwa za kuwakomboa Watanzania kuondokana na changamoto zinazowakabili.

"Kwa miaka mingi, nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na changamoto katika eneo la huduma za afya,elimu miundombinu, umeme, kilimo na katika masuala yanahusu utawala bora." anasema.

Anasema,Serikali ya awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia kwa kipindi cha miaka mitatu imeweka jitihada kubwa kukwamua eneo la miundombinu.

Taifa limepiga hatua kubwa za maendeleo kwa kujenga, kukarabati na kufungua barabara mpya katika maeneo mengi hususani vijijini.

"Vipo vijiji ambavyo havikuwa vinafikika lakini kwa sasa vinafika kwa kuwa jitihada kubwa zimeekezwa kuhakikisha barabara mpya zinafunguliwa maeneo yote nchini ambako watanzania wanaishi."

Anaongeza kusema kuwa miundombinu ya barabara ina umuhimu mkubwa katika kuchochea maendeleo hasa ukizingatia kuwa wengi wa watanzania ni wakulima hivyo miundombinu inayo boreshwa itawasaidia kuweza kuyafikia masoko kiurahisi na kuzifikia buduma nyingine za kijamii kiurahisi.

Anatolea mfano kuwa yapo maeneo akina mama wajawazito walikuwa wanajifungulia njiani na wengine kufa kwa kutokana na ama ubovu au ukosefu wa miundombinu ya barabara kuelekea kwenye huduma za afya.

Hamoud anasema kuwa miaka mitatu ya Rais Samia madarakani anaiona kama miaka 30 kwa kuwa mambo yaliyofanyika ni mengi kwa kulinganisha na muda mfupi aliokaa madarakani.

" Mathalani, katika eneo la afya.Ni ukweli usiopingika huduma za afya zimeboreshwa kwa kiwango kikubwa. Ukarabati wa hospitali za rufaa na ujenzi wa hospitali za mikoa, wilaya, zahanati na vituo vya afya, ni eneo ambalo Rais Samia ametia fora."anasema.

Anaongeza kusema kuwa hospitali hizo hazikuishia kwenye kufanyiwa ukarabatiwa na kujengwa bali zimewezeshwa kupata mashine za kisasa kama vile CT SCAN, MRI na mashine nyingine kwa ajili ya vipimo vikubwa na vidogo, dawa na watoa huduma.

" Moja ya changamoto ambayo imekuwa ikiwakabili watanzania ni huduma duni za afya. Jitihada za Rais Samia katika kuboresha eneo hilo la huduma za afya ni kubwa ambazo ninaamini katika kipindi kifupi kijacho changamoto hiyo itabaki historia." anasema.

Akizungumzia ukuaji wa sekta ya kilimo,Hamoud anasema kuwa asilimia 65 ya watanzania ni wakulima, hivyo kilimo ni sekta inayoajiri watu wengi.Jitihada za serikali ya awamu ya sita kuboresha kilimo ni wazi kuwa zimelenga kubadili hali ya maisha ya kundi kubwa la watanzania.

" Pamoja na mambo mengine mengi, katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia madarakani tumeona kuwa bajeti ya kilimo imepaa mara dufu.Lengo kuu ni kuboresha sekta hii muhimu na kuhakikisaha kuwa kundi kubwa la Watanzania wanakuwa na chakula cha kutosha pamoja na kipato cha uhakika." anasema.

Hamoud anaongeza kusema kuwa hatua ya serikali ya awamu ya sita kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima imechangamsha sekta ya kilimo na kutoa hamasa kwa kundi kubwa la watu kushiriki shughuli za kilimo.

" Bei ya mazao ya kilimo kwa kipindi cha awamu hii ya sita, imekuwa ni bei rafiki na yenye maslahi kwa wakulima. Wakulima wanalima na kuuza mazao yao kwa bei nzuri na pia wapo huru kupeleka mazao hayo sehemu yoyote kwa lengo la kufuata bei yenye maslahi zaidi." anasema.

Anasema,hatua hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kuyaboresha maisha ya wakulima huku idadi kubwa ya vijana ikijiingiza kwenye sekta ya kilimo.

" Sera nzuri za kilimo imechangia kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuboresha maslahi ya mkulima, hatua ambayo imewavutia vijana wengi kuamua kujiajiri katika sekta ya kilimo na kuwaondolea adha ya kukosa ajira." anasema Hamoud.

Anasema kuwa serikali ya awamu ya sita imeboresha sekta nyingi ikiwemo sekta ya elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa kwa wingi hivyo kuwaondolea watoto wetu adha ya kusomea chini ya miti na kutembea umbali mrefu kufuata shule.

" Miaka mitatu ya Rais Samia imebadili taswira ya elimu Tanzania. Imeboresha miundombinu ya utolewaji wa elimu na maslahi ya walimu.

Unaweza ukaboresha miundombinu tu ukaacha kuboresha masalahi ya walimu, lakini Rais Samia, amefanya yote kwa pamoja ikiwa ni kuboresha miundombinu na maslahi ya walimu jambo ambalo ni msingi mkubwa wa utolewaji wa elimu bora." anaeleza Hamoud.

Akizungumzia kuhusu utawala bora Hamoud anasema kuwa R4 za Rais Samia ni ubunifu wa hali ya juu ambao unaimarisha utawala bora, amani, udugu na mshikamano wa kitaifa.

Hivyo anaamini kuwa jitihada zinazofanyika katika kuimarisha sekta za maendeleo, sambamba na R 4 ambazo kimsingi zinaimarisha utawala bora, safari ya watanzania kuelekea nchi ya ahadi inakaribia kufika.





# TWENDENI TUKALISOME AZIMIO LA ARUSHA

NA MWANDISHI WETU

WAKATI wa uhai wake, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kulalamika kuona jinsi misingi ya Azimio la Arusha ilivyokuwa inasiginwa.

Mwalimu aliwahi kusema katika moja ya mikutano yake na Waandishi wa Habari akisema katika maisha yake hakuwahi kuona ni wapi Azimio la Arusha lilikosewa.

Baba huyo wa Taifa alikuwa akiitetea misingi ya Azimio la Arusha, ambalo pamoja na mengine lilikuwa na misingi ambayo ilikuwa imeweka miiko kwa viongozi.

Mojawapo ya miiko ya Azimio hilo la mwaka 1967, ilikuwa ni kuwazuia viongozi kuwa wafanyabiashara wakati wakiwa madarakani.

Hadi Mwalimu anang'atuka madarakani mwaka 1985, bado kulikuwa na woga kwa viongozi kufanya biashara, na ilitafsiriwa wakati ule kwamba kiongozi kuwa mfanyabiashara kungemfanya kumiliki mali nyingi, na huo ulikuwa ni sawa na ubepari.


Lakini baada ya hapo, sheria mbalimbali zilibadilika na mabadiliko ya kisera na kiuchumi duniani kote yakaifanya Tanzania kuwa nchi ambayo mambo mengi yalianza kufanywa nje ya misingi hiyo ya Azimio ka Arusha.

Utandawazi ambao ulikuja na kasi ya soko huria ukaondoa moja kwa moja vikwazo na miiko ambayo ilikuwa inawaba viongozi, na kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 90, viongozi wengi walikuwa wakimiliki mali nyingi, na kusema ukweli wakaanza kuingia kwenye biashara moja kwa moja.

Pamoja na sheria ya kuwataka kutaja mali zao, lakini sheria hiyo haiwakatazi kufanya biashara moja kwa moja, lakini inawataka kuorodhesha mali zao wanapoingia madarakani.

Madhara ya kulegeza masharti kwa viongozi, ni makubwa kuliko ambavyo ilitarajiwa pengine. Haikuwa rahisi huko nyuma viongozi kununua uongozi kwa maana ya kuhonga wapiga kura, lakini leo kuna viashiria kwamba maeneo mbalimbali katika nchi hii, viongozi wetu wameingia madarakani kwa kununua uongozi.

Wamenunua uongozi kwasababu wanajua kwamba kupitia nafasi wanazokwenda kukamata, watapata nafasi ya kufanya biashara mbalimbali, na pesa wanazotumia kununua




uongozi zitarudi.V Kwa lugha moja ama nyingine, uongozi kwa baadhi ya watu umekuwa ni biashara yenye faida kubwa.

Haishangazi leo kusikia Mkuu wa Wilaya, au Mkoa anaacha nafasi hiyo kwenda kugombea Ubunge akiamini kwamba kwenye ubunge kuna mshahara mkubwa na posho nyingi za vikao kuliko kwenye Ukuu wa Wilaya au Mkoa.

Lakini Mbunge, ana uhakika wa kubaki madarakani kwa miaka mitano, na akiaminika zaidi na wananchi wake hata miaka miaka 10 na zaidi, kuliko Ukuu wa Wilaya au Mkoa, nafasi ambayo Rais akiamua anaweza kukunyang'anya wakati wowote.

Sitaki kugusia maslahi ya waheshimiwa wabunge kwa undani zaidi, lakini kila Mtanzania mwenye akili timamu anajua kwamba waheshimiwa wabunge wanaishi maisha mazuri kuliko viongozi wengine wa kuteuliwa katika ngazi za mikoa na wilaya.

Leo hii wakati wananchi wanalalamika kuhusu ugumu wa maisha katika baadhi ya maeneo, kuna viongozi wao wamekuwa wakifanya biashara ambazo moja kwa moja zinawaumiza wananchi hao.

Kwa mfano, kama kiongozi anamiliki kampuni ya mafuta kwa mfano, anawezaje kusimama kwenye jukwaa lolote la kisiasa ama kijamii kupigania bei ya mafuta ishuke?

Miiko ya Azimio la Arusha ilisaidia sana kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye heshima. Sio kwamba leo hii taifa letu linaweza kujikuta linapoteza heshima heshima, lakini ile misingi ya utawala bora inaweza kuvurugwa kwa kiasi kikubwa.

# TAKUKURU SHIKILIENI HOJA YA DK.MPANGO



NA MWANDISHI WETU

**HATIMAYE mwaka wa uchaguzi umewadia. Joto tayari limepanda kila kona.Vyama vya siasa vimeshaanza kujiwinda na kinyang'anyiro hicho kitakachopulizwa kipyenga Oktoba mwaka huu.**

Tayari Chama cha Mapinduzi(CCM) kimeshapata mgombea wake wa Urais ambaye ni Dk.Samia Suluhu Hassan ambaye amepitishwa kwa kishindo na Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama hicho.

Mgombea mwenza wake ni Dk.Emmanuel Nchimbi ambaye amechukua mikoba ya Dk,Philip Mpango aliyemuandikia Rais Samia barua kuomba kupumzika majukumu ya kisiasa.

Ukiacha CCM kule ACT Wazalendo nako mambo ni moto kwani pazia la kutangaza nia ya kugombea nafasi mbalimbali kupitia tiketi ya chama hicho sasa kila kitu kipo hadharani. Kule CHADEMA mchakato wa uchaguzi wa Taifa ndani ya chama hicho umepamba moto leo watapata viongozi wapya.

Wakati hali ikiwa hivyo lakini ndiyo kipindi ambacho mianya ya rushwa hupata nafasi kwa wagombea kuwanunua wapiga kura katika mchakato wa ndani lakini pia hata wakati wa uchaguzi wenyewe.

Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango, kwakutambua hili ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kujiandaa kikamilifu kukabiliana na kudhibiti vitendo vya rushwa katika Uchaguzi Mkuu mwaka huu, huku akiitaka kuangazia zaidi kwenye matumizi ya mitandao na simu katika kuhamisha pesa za rushwa.

Makamu wa Rais anasema ni muhimu TAKUKURU kujizatiti kupambana na vitendo hivyo vya rushwa ambavyo vina madhara makubwa kwa maendeleo ya Taifa kwa kuwa Viongozi wanaochaguliwa kwa njia ya rushwa hawawezi kukemea vitendo vya rushwa, kutatua kero za wananchi pamoja na kusimamia vema miradi ya maendeleo.

Dkt. Mpango anasema,lazima viongozi na watumishi wa TAKUKURU kuwa mfano wa kuigwa kwa mienendo mizuri, kufuatilia tuhuma mbalimbali kwa umakini na bila upendeleo. Anaongeza kwamba ni muhimu kufanya maamuzi kwa haki na kutumia madaraka kutatua kero za wananchi kwa manufaa ya umma na siyo binafsi.

Makamu wa Rais anaitaka TAKUKURU kuzingatia kufanya kazi kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu, kujituma na kutanguliza maslahi ya Taifa mbele ili Taasisi hiyo iwe na ufanisi.

Dkt. Mpango amesema, ni vema kuimarisha mifumo ya kuchunguza, kuzuia na kuadhibu wanaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa kwa mujibu wa sheria.

Amesisitiza ofisi zote za TAKUKURU nchini kuunganishwa na mifumo ya TEHAMA pamoja na kuwajengea uwezo na mbinu za kisasa za uchunguzi na uendeshaji wa kesi za rushwa watumishi wa TAKUKURU wanaotekeleza jukumu la kuzuia na kupambana na rushwa.

Amesisitiza suala la watumishi wa TAKUKURU wanaotekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria na kanuni, pamoja na watoa taarifa kutambuliwa na kulindwa wawapo kazini au nje ya kazi, ili kuepuka kuhatarisha maisha yao.

Aidha, ametoa wito kwa vyombo vya habari kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa kwa kuelimisha jamii, kuandika taarifa za kiuchunguzi ili kufichua vitendo vya rushwa na kusaidia vyombo vya dola kufanya kazi yake.

Amesema kitendo cha baadhi ya vyombo vya habari kudaiwa kutumika kupotosha habari au kutoa habari zenye mrengo fulani, kinaweza kuwa na madhara makubwa katika jamii kwa kuikosesha jamii haki ya kupata habari ambazo zinaweza kuwa na manufaa katika mapambano dhidi ya rushwa.

Ametoa wito kwa Mkutano huo kutumika kubuni mbinu na mikakati ya kukabiliana na rushwa katika mahakama za chini, mabaraza ya ardhi, na vyombo vingine vya haki jinai ili kuhakikisha wananchi wanapata haki zao.

Ameisisitiza TAKUKURU kutekeleza agizo la kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya wasimamizi wa miradi watakaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa au ubadhirifu katika miradi iliyobainishwa wakati wa Mbio za Mwenge 2024.

Makamu wa Rais amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kuwekeza katika ujenzi wa Taasisi imara za haki jinai ili kupambana na makosa ya jinai ikiwemo rushwa.

Amesema Serikali itaendelea kuiwezesha TAKUKURU kwa upande wa rasilimali fedha na rasilimali watu ili kutekeleza wajibu wake wa kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Crispin Chalamila amesema kutokana na uwezeshaji uliyofanywa na Serikali kwa Taasisi hiyo, katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kiasi cha shilingi bilioni 18 kimeokolewa kupitia operesheni mbalimbali za uchunguzi pamoja na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo.


Amesema Fedha hizo zilirejeshwa serikalini na nyingine kutumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kadri ilivyokusudiwa.

Aidha amesema kwa kipindi cha miezi 12, TAKUKURU inajivunia mafanikio ya ushindi wa Jamhuri wa asilimia 75.5 katika kesi zilizotolewa maamuzi ikilinganishwa na asilimia 67.7 ya ushindi wa kesi zilizotolewa maamuzi mwaka 2023.

Ameongeza,TAKUKURU imeendelea na jukumu lake la kuelimisha umma kuhusu madhara ya rushwa na kuhamasisha umma kushiriki mapambano dhidi ya adui rushwa kupitia njia mbalimbali kama vile mikutano, minada, midahalo, semina, warsha, Mbio za Mwenge wa Uhuru, vipindi vya redio, televisheni na machapisho mbalimbali.



# Virusi vya Marburg ni nini?



**RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk.Samia Suluhu Hassan amethibitisha uwepo mgonjwa mmoja mwenye maambukizi ya virusi ya ugonjwa wa Marbug. Awali kulikua na tetesi za uwepo wa ugonjwa huo Mkoani Kagera na kwamba umesababisha vifo vya watu nane jambo ambalo halikuwa na ukweli.**

Taarifa ya Shirika ya Shirika la Afya Duniani(WHO)iliyochapishwa mtandaoni ilisema kuwa mnamo Januari 10 mwaka hu ilipokea ripoti za kuaminika kutoka kuhusu visa vinavyoshukiwa vya ugonjwa huo katika mkoa wa Kagera.Dalili za ugonjwa huo ni pamoja na kikohozi, maumivu ya viungo, kuhara na kutapika, na mara nyingi hata upungufu wa damu katika mwili.

Ugonjwa wa Marburg ni nini?

Kulingana na Umoja wa Mataifa, virusi vya Marburg, ambavyo ni sawa na virusi hatari vya Ebola, viligunduliwa kwa mara ya kwanza baada ya watu 31 kuambukizwa, saba kati yao walikufa, mnamo 1967 huko Marburg na Frankfurt. Ujerumani na Belgrade huko Serbia.

Virusi vya Marburg vilipatikana kwa mara ya kwanza kwa tumbili wa kijani kibichi wa KiafrikaChanzo cha picha,Getty Images

Maelezo ya picha,Virusi vya Marburg vilipatikana kwa mara ya kwanza kwa tumbili wa kijani kibichi wa Kiafrika

Mlipuko huo ulitokana na tumbili wa Kiafrika walioagizwa kutoka Uganda. Lakini virusi hivyo vimehusishwa na wanyama wengine tangu wakati huo.

Na miongoni mwa wanadamu, huenezwa zaidi na watu ambao wamekaa kwa muda mrefu katika mapango na migodi iliyo na popo.Huu ni mlipuko wa kwanza nchini Ghana - lakini nchi kadhaa za Afrika zimewahi kuripoti mlipiko wa virusi ikiwa ni pamoja:

Mlipuko wa mwaka 2005 nchini Angola ulisababisha vifo vya watu zaidi ya 300. Lakini barani Ulaya, ni mtu mmoja tu amefariki katika kipindi cha miaka 40 - na mmoja nchini Marekani,baada ya kurejea kutoka katika safari ya kuzuru mapango nchini Uganda.

Milipuko mikubwa:

2017, Uganda: visa vitatu, watu watatu walifariki 2012, Uganda: vis 15, watu wanne walifariki

2005, Angola: visa 374, watu 329 walifariki

1998-2000, DR Congo: visa 154 cases, watu 128 walifariki

1967, Ujerumani: visa 29, watu saba walifariki

Chanzo: WHO

Inasababisha ugonjwa gani?

Unaanza ghafla na:Homa kuumwa vibaya na kichwa

kuumwa na misuli Hii mara nyingi siku tatu hufuatwa na:kuharisha

kuumwa na tumbo kichefuchefu na kutapika.

WHO inasema: "Mwonekano wa wagonjwa katika awamu hii umeelezewa kuwa unaonyesha sifa za 'kama mzimu', macho ya ndani, nyuso zisizo na hisia na uchovu mwingi."

Baadhi ya watu hutokwa na damu sehemu mbalimbali za mwili na kufa siku nane hadi tisa baada ya kuugua kwa sababu ya kupoteza damu nyingi na mshtuko.Kwa wastani, virusi huua nusu ya walioambukizwa, WHO inasema, lakini aina hatari zaidi imeua hadi 88%.

Popo wa matunda wa rousette wa Misri ndiye mbebaji mkuu wa

Je, inaeneaje?Popo wa matunda aina ya rousette wa Misri mara nyingi huwa na virusi. Nyani wa kijani kibichi na nguruwe wanaweza pia kubeba.

Miongoni mwa wanadamu, huenea kupitia maji ya mwili na malazi yaliyochafuliwa nao. Na hata watu wakipona, damu au shahawa zao, kwa mfano, zinaweza kuwaambukiza wengine kwa miezi mingi baadaye.

Je, inaweza kutibiwaje?

Hakuna chanjo maalum au matibabu ya virusi.

Lakini aina mbalimbali za bidhaa za damu, madawa ya kulevya na matibabu ya kinga yanatengenezwa, WHO inasema.Na madaktari wanaweza kupunguza dalili kwa kuwapa wagonjwa waliofika hospitali maji mengi ili kuchukua nafasi ya damu iliyopotea.

Vinawezaje kudhibitiwa?

Watu barani Afrika wanapaswa kuepuka kula au kushika nyama ya porini, Gavi, shirika la kimataifa linalokuza upatikanaji wa chanjo, linasema.Watu pia wanapaswa kuepuka kuwa karibu na nguruwe katika maeneo yenye mlipuko, WHO inasema.


Wanaume ambao wamekuwa na virusi wanapaswa kutumia kondomu kwa mwaka mmoja baada ya kupata alili au hadi shahawa zao zitakapothibitishwa mara mbili kuwa hazina virusi.Na wale wanaozika watu ambao wamekufa kutokana na virusi wanapaswa kuepuka kugusa mwili.

# WANAOTAFUTWA

NA CHARLES MATESO
MOHAMMED DEIF:

**'MGENI' ASIYEJUA PA KULALA, ISRAEL WANAMLILIA**

KWELI MAGAIDI? Unaweza kujiuliza juu ya Hamas, ambao Marekani na baadhi ya washirika wake wanaliita hivyo na hata viongozi wake kuwekwa katika orodha ya magaidi, lakini huo ndiyo ukweli wa mambo?



**Mohammed Al-Deif**

Kuna siku tutaingia kwa undani zaidi kuhusu hilo, lakini Hamas ni chama cha kisiasa, ambacho kinaingia katika chaguzi na kupigiwa kura kama kawaida, ila msimamo wake juu ya Israel na kutaka taifa huru la Palestina ndio umewafikisha huko.

Viongozi wake wanalengwa mno na Israel na washirika wake, ndiyo maana hata kuuawa kwa naibu kiongozi wa kundi hilo, Saleh al-Arouri mjini Beirut, Lebanon mwanzoni mwa mwaka huu kulisababisha maandamano makubwa Ramallah.

Mkuu wa Hamas, Ismail Haniyeh aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Palestina ambaye aliuawa na Israel mapema mwaka huu, aliwahi kukaririwa akisema mauaji hayo pia ni ukiukaji wa mamlaka ya Lebanon na unachochea uadui wa Palestina na Israel.

Katika hotuba yake iliyopeperushwa kwenye televisheni, Haniyeh alimuomboleza al-Arouri na viongozi wawili wa Brigedi za Al Qassam, Samir Findi Abu Amer na Azzam Al-Aqraa Abu Ammar.

Viongozi wote hao waliuawa katika shambulio la ndege zisizo na rubani za Israel katika viunga vya Beirut kusini mwa Dahiyeh. Hata Ismail Haniyeh, kabla ya yeye kuuliwa, alikutana na machungu haya kwa familia yake pia kuuawa.

Aprili 2023, Hamas ilitangaza kwamba watoto watatu na wajukuu wanne wa Ismail Haniyeh, kiongozi wa kundi hilo waliuawa katika shambulio la anga katika kambi ya wakimbizi ya Shati huko Gaza, ambapo familia iliwatembelea jamaa zao wakati wa sherehe za Eid al-Fitr.

**Mohammed Al-Deif Ni Nani?**

Alizaliwa mwaka 1965 na kuitwa jina la Mohammed Diab Ibrahim al-Masri. Alizaliwa ndani ya Kambi ya Wakimbizi ya Khan Yunis iliyopo Gaza, ambayo ilianzishwa mwaka 1948 baada ya Vita vya Palestina.

Inadaiwa aliacha shule kwa muda ili kupambana kuilisha familia yake, ambayo ilikuwa katika hali mbaya kiuchumi, ila alifanikiwa kupata Shahada ya Kemia kutoka Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Gaza mwaka 1988.

Masri alijiunga na Hamas mwaka 1987 na kujulikana kwa jina la Mohammed Deif, likiwa na maana ya 'mgeni' kwa lugha ya Kiarabu, lakini hii ni kutokana na aina ya mfumo wa kuishi aliokuwa nao.

Israel wakiongozwa na Marekani wanadai Deif kati ya miaka ya 1990 na 2000, aliongoza mashambulizi kadhaa ya watu kujitoa muhanga, ikiwemo lile la mwaka 1996 la kulipua basi katika Barabara ya Jaffa Road.

Alikuja kuongoza kikosi cha al-Qassam mwaka 2002 na Israel inadai alibadilisha muundo mzima wa brigedi hiyo hadi kuwa kikosi kamili cha jeshi na kilicho hatari zaidi.

Israel ilidai mashambulizi yote ya roketi yaliyokuwa yakielekezwa kwao yalichangiwa na 'akili za mtu huyu', huku ikidai alihusika zaidi na shambulizi la Oktoba 2023 ndani ya Israel ambalo limesababisha vita kati yao mpaka sasa.

Israel imemuorodhesha kati ya mtu anayesakwa zaidi toka mwaka 1995 na ishapanga kumuua mara kadhaa, lakini kote huko imeshindwa na amefanikiwa kuponyoka katika majaribio saba ya kumuua. Mwaka 2014 ndege za Israel zilimuua mkewe na mtoto wake wa kike wa miaka mitatu.

**The Mastermind**

Al-Deif anadaiwa ni mtaalamu wa ujenzi wa mahandaki yaliyofanikisha wapiganaji wa Hamas kuingia ndani ya Israel wakitokea Gaza, hivyo kusababishwa kupachikwa jina la 'The Mastermind', akiwa anaongoza Brigedi za Izz al-Din al-Qassam, ambalo ni tawi la kijeshi la Hamas.

Kutokana na kukwepa kwake kifo Waisrael wamempachika jina la 'The Man of Death' au 'The Fighter with Nine Lives', lakini awali alikuwa akipenda sana sanaa ya uigizaji na alishawahi kuunda kikundi chake.

Israel ilishawahi kumkamata mnamo mwaka 1989 na kumuweka gerezani kwa miezi 16 bila kumpeleka mahakamani, kwa tuhuma za kufanya kazi na kitengo cha jeshi cha Hamas.

Lakini aliwekwa katika orodha ya kusakwa na Israel mwaka 1996 kwa madai ya kusimamia operesheni za kulipiza kisasi ya mauaji ya Yahya Ayyash, ambapo yalisababisha Waisraeli wapatao 50 kufa.

Akamatwa atoroka


Israel ilimkamata na kumtia gerezani mwaka 2000 kwa kamadai ya mauaji ya askari watatu miaka ya 1990, lakini alifanikiwa kutoroka na kuwaacha wengi mdomo wazi.

Zilipopitiwa picha za kamera ilionekana watu watatu wakiingia na kutoka, moja ikimuonesha mtu mmoja aliye mno akiwasindikiza watu wawili na aanamika alikuwa mmoja wao.

**Mikakati Jeshini**

Deif alijiunga na Hamas mwaka 1987 wiki kadhaa baada ya kile kilichojulikana kama 'Intifada ya Kwanza', lakini alikamatwa na alipokuja kuachiliwa aliposhikiliwa kwa miezi 16 alisaidia kuanzishwa kwa Izz ad-Din al-Qassam Brigades, tawi la kijeshi la Hamas. Itaendelea





# DIDDY

## FROM MANSION TO CUBBYHOLE

KUANZIA muvi ya "Straight Outta Compton" hadi andiko la kitaaluma (dissertation) la Kristen Bowen, Chuo Kikuu cha North Carolina. Documentaries za "In The Dark", "Surviving Diddy" kisha "Freak Off Parties". Halafu kitabu "Mercedes Ladies" cha Sherri Sher.

Kila moja inatosha kujenga picha ya mwanzo wa mwisho wa binadamu ambaye alipata kuwa kila kitu katika ulimwengu wa burudani. Sean Combs "Diddy", zamani "P Diddy". Miaka ya 1990, aliitwa "Puff Daddy" au simply "Puffy".

Muvi ya Straight Outta Compton, inasimulia maisha halisi ya vijana watatu wenye vipaji na fedha kutoka Compton, California; Eazy E, Ice Cube na Dr Dre. Walikuwa memba wa Hip Hop crew ya N.W.A (Niggaz Wit Attitudes). "Straight Outta Compton" ni albamu yao ya kwanza na iligonga platinum mwaka 1988.

Ndani ya movie ya Straight Outta Compton, kilichowasilishwa kama uhusika wa Eazy, Cube na Dre, ndicho kimeandikwa na Kristen katika dissertation (tasnifu) yake yenye jina "Sexual Violence, Black Survivors, and Moving Beyond Resilience."

N.W.A, baada ya kufanya vizuri sokoni, utawaona wakiangusha house parties za nguvu. Humo ni pombe, wanawake na bangi. Mapenzi kwa makundi. Mastaa watatu katikati ya msitu wa wanawake. Uchafu wa kila aina unafanyika. Huoni thamani ya mwanamke zaidi ya kuwa chombo cha starehe.

Wanawake wote ni Weusi. Hili linafafanuliwa na Kristen katika tasnifu yake chuoni North Carolina, kwamba wanawake weusi kutumikishwa kingono ni mnyororo wa kihistoria tangu zama za utumwa. Kisha, utamaduni maarufu (popular culture), mwanzoni ulitawaliwa na Wazungu kibiashara.

Kutokana na hali hiyo, Wazungu waliwazubaisha mastaa Weusi kwa kuwaandalia parties zenye pombe na wanawake. Fedha zao nyingi zilipotea humo. Ndicho kinachoonekana kwenye muvi "Straight Outta Compton", na ni moja ya sababu za kusambaratika kwa N.W.A mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Parties hizo za pombe na wanawake Weusi, zinashabihiana na Freak Off Parties za Diddy, vilevile mnyororo wa mastaa Weusi, kukumbwa na kashfa nyingi za kuwanyanyasa kingono wanawake Weusi, hadi ubakaji. Diddy akaunga orodha. Hatimaye yupo nyuma ya nondo.

Mwaka 1993, Rapa Tupac Shakur, alitoa ngoma "Keep Ya Head Up", ambayo iligeuka wimbo pendwa kwa kila mwanamke Mweusi. Katika single hiyo, Tupac anawashukia vikali wanaume Weusi, tabia yao ya kubaka wanawake. Alipokuwa hai, Tupac alisema, aliandika wimbo kwa sababu vitendo vya ubakaji kwa wanawake Weusi vilikuwa vingi na wabakaji ni wanaume Weusi.

Oktoba 1999, ikiwa ni miaka mitatu tangu kifo cha Tupac, ulitolewa wimbo mwingine wa rapa huyo, unaoitwa "Baby Don't Cry", ambao ni sehemu ya pili ya "Keep Ya Head", akifikisha ujumbe jinsi wanawake Weusi wanavyonyanyaswa kingono kwa kubakwa hovyo na wanaume Weusi.

Sherri, mwasisi wa kundi la Mercedes Ladies, ambalo ni Hip Hop squad ya kwanza ya wanawake Marekani na duniani, kupitia kitabu chake "Mercedes Ladies", amesimulia kama hadithi ugumu wa wanawake kwenye tasnia ya burudani.

Kuanzia alivyobakwa na guardian wa Hip Hop, Russell Simmons, hadi vikwazo ambayo yeye na wenzake walipitia kila hatua, wakishurutishwa watoe rushwa za ngono. Mstari wa Solo Thang, "binti kulala kwa prodyuza" au line ya Dataz "binti kupromotiwa kimuziki na kimwili." Ndiyo hali Mercedes Ladies waliipitia. Sherri amesimulia.

**HATIMA YA DIDDY**

Diddy, mwana-Hip Hop tajiri ambaye mwishoni mwa miaka ya 1990 hadi katikati ya muongo wa pili wa miaka ya 2000, alitambulika kama mwanamuziki mwenye fedha nyingi zaidi duniani, kabla ya kupitwa na Jay Z, kisha Kanye West na Rihanna.

New York finest, Diddy, ni mtetezi hasa wa jumuiya ya watu Weusi. Alianzisha slogan ya kukweza mafanikio ya watu Weusi, aliyoiita "Black Excellence". Zaidi, Diddy, alikuwa kiunganishi cha watu Weusi maarufu na mpatanishi palipo na migogoro. Hata hivyo, hivi sasa ni kama anaielekea omega!..itaendea

KUMEKUCHA MICHEZO
Tovuti: www.kumekucha.co.tz

# RAMOVIC ASHITUKIA MCHEZO

## Awaweka kitimoto mastaa Yanga



NA ILHAM JUMA

**KITENDO cha Yanga kushindwa kufuzu robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAF CL), imezua jambo. Kocha wa Yanga, Sead Ramovic amewajia juu wachezaji wake, pia akifumua programu ya mazoezi ya kikosi hicho.**

Wikiendi iliyopita Yanga ilishindwa kupata matokeo dhidi ya MC Alger ya Algeria, kitendo cha kufelishwa kufuzu robo fainali ya michuano hiyo toka Kundi A, licha ya Wananchi kuwa na imani kubwa.

Sasa, kutokana na kufeli huko, kocha huyo raia wa Ujerumani ameonesha kukerwa nayo, hivyo amekuja na mbinu mbadala ili Wananchi warejeshewe furaha zao.

Katika kikao chake na wachezaji baada ya dakika 90 za mechi hiyo, Ramovic aliwaeleza walivyomkera kwa nafasi nyingi za wazi walizoshindwa kuzitumia kufunga mabao.

Gazeti hili linafahamu kuwa kikao hicho kilichukua takribani dakika 45, ambapo kocha huyo kuwaeleza wachezaji wake kuwa uzembe waliofanya umewakasirisha mashabiki, hivyo hawapaswi kurudia.

"Alionekana amekasirika. Aliitupia lawama safu ya ushambuliaji, ingawa hakuwa akitaja jina la mchezaji," kilisema chanzo kilichopiga stori na KUMEKUCHA SPOTI.

Kwa upande mwingine, Ramovic amebadili programu ya kikosi hicho, ambapo sasa ameamua kuongeza muda wa mazoezi ya timu hiyo.

Awali, tizi la Yanga katika Uwanja wa Avic Town, Kigamboni, jijini Dar es Salaam, lilikuwa linachukua saa mbili na nusu hadi tatu.

Lakini, mabadiliko ya Ramovic baada ya kile kilichotokea Jumamosi yatawafanya wachezaji wahenyeke mazoezini kwa saa tatu hadi nne.

Gazeti hili limebaini kuwa mabadiliko hayo yametokana na raia huyo wa Ujerumani kuanza kuichungulia mechi zilizopo mbeleni, ambapo Jumamosi watacheza mechi ya Kombe la Shirikisho la CRDB, wakicheza dhidi ya Copco, akiamini mechi hiyo itarejesha morali kwenye kikosi chake.

# SIMBA YATOA KAULI YA KIBABE CAF

NA MOHSIN JUMA

WAWAKILISHI wa Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika Simba wametangaza kauli ya kibabe kwa wapinzani wao watakaopangiwa nao katika hatua ya robo fainali wakisema ni mwendo wa vichapo hadi fainali.

Simba ilimaliza mechi za hatua ya makundi kibabe kwa kuongoza kundi A mbele ya Waarabu CS Costantine na sasa inasubiri kupangiwa wapinzani wake katika mechi za robo fainali ili kuanza upya vita ya kutimiza ndoto za kucheza fainali ya michuano hiyo.

Kwa mujibu wa Msemaji wa klabu hiyo,Ahmed Ally,wako tayari kupangiwa na timu yoyote ili waendeleze moto waliouanza katika mechi za hatua ya makundi.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), mechi za robo fainali zitachezwa mwishoni mwa Machi hadi mwanzoni mwa Aprili mwaka huu.

Simba imetinga robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kama vinara wa Kundi A wakiwa na pointi 13, wakifuatiwa na CS Constantine ya Algeria wenye pointi 12.

Sasa miamba nane iliyotinga robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, Februari ama mwanzoni mwa Machi, itajua kila mmoja ametupwa kucheza na nani, huku wawakilishi pekee wa Tanzania katika michuano hiyo ikiwa na kiu ya kumfahamu mpinzani wake.

Kuelekea droo hiyo Simba hawana mchecheto kwani si wageni wa michuano hiyo, hivyo kwa kauli moja wanamsubiri yeyote atakayepangwa ili wajue namna ya kumsambaratisha.

Kiburi hicho cha Wekundu hao wa Msimbazi msimu huu, kinakuja kutokana na ubora wa kikosi chao ambacho kimesheheni mastaa wa daraja la juu wakinolewa na Kocha Fadlu Davids.

Lakini Simba ndio timu ambayo inapewa upatu wa kubeba kombe hilo, kutokana na ukubwa waliokuwa nao katika michuano ya CAF miaka ya hivi karibuni.

